



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

P. O .Box 796, Tel: +255 (0) 22-2122722/3, Fax: +255 (0) 22-2130852
Dar es Salaam, TANZANIA, E-mail: dg@nbs.go.tz



Kumb Na: NBS/C.30/4

Tarehe: 07 Januari 2014

YALIYOJITOKEZA

FAHIRISI ZA UZALISHAJI WA BIDHAA ZA VIWANDANI KWA MWAKA 2012

Maana ya Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani

Fahirisi za uzalishaji wa bidhaa za viwandani hupima mabadiliko ya kiasi cha bidhaa zilizozalishwa na wazalishaji mbalimbali ambao kwa wastani wameajiri kuanzia wafanyakazi 50 na kuendelea. Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani hutolewa kwa kila robo mwaka na kwa mwaka.

Utoaji wa fahirisi hizi ni mwanzo na muendelezo wa kusambaza takwimu za Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani kwa wadau.

Makundi ya Bidhaa

Bidhaa za viwandani zimewekwa katika makundi mbalimbali kwa kufuata mwongozo wa Umoja wa Mataifa "*United Nations International Standard Industrial classification Rev 3 of all economic activities*". Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani zimetolewa katika makundi manane ambayo ni 1) Chakula, vinywaji na tumbaku; 2) Nguo na ngozi; 3) Mbao na bidhaa za mbao; 4) Karatasi na bidhaa za karatasi; 5) Madawa, petroli na bidhaa za plastiki; 6) bidhaa za udongo, vioo na bidhaa zisizo za metaliki; 7) Viwanda vya chuma; na 8) Bidhaa zitokanazo na chuma.

Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani

Ukokotoaji wa fahirisi umefanyika kwa kufuata kanuni ya "*Chained Laspeyre's*" badala ya kanuni ya kawaida yaani "*Laspeyre's fixed base*" ili kujumuisha mabadiliko yanayotokea katika uzalishaji wa bidhaa za viwandani nchini.

Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani


Katika mwaka 2012, fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani ulikuwa ni 328 ikilinganishwa na 296 kwa mwaka 2011 ambayo ni ongezeko la asilimia 10.8. Ongezeko hili limechangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa katika makundi ya vyakula, vinywaji na tumbaku (16.8 asilimia); na viwanda vya chuma (14.6 asilimia). Hata hivyo bidhaa za nguo na ngozi zimeongezeka kwa asilimia hasi (17.7 asilimia) kama inavyonekana kwenye Jedwali namba 1.

Jedwali namba 1: Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani

Makundi ya Bidhaa za Viwandani	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	Badiliko katika asilimia 2011-2012
Chakula, Vinywaji na tumbaku	314	324	351	375	386	392	458	16.8
Nguo na ngozi	271	268	286	229	244	226	186	-17.7
Mbao na bidhaa za mbao	256	331	263	246	244	373	374	0.3
Karatasi na bidhaa za karatasi	74	198	310	295	317	343	360	5.0
Kemikali, Petroli na Bidhaa za plastiki	96	99	107	125	137	140	129	-7.9
Bidhaa za udongo, vioo na bidhaa zisizo za metaliki	320	395	415	459	526	536	576	7.5
Viwanda vya chuma	135	143	177	191	235	260	298	14.6
Bidhaa zitokanazo na chuma	56	61	74	72	76	82	91	11.0
Jumla-Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani	226	238	260	274	290	296	328	10.8
Badiliko katika asilimia		5.3	9.2	5.4	5.8	2.1	10.8	

Katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2012 kiwango cha juu cha mabadiliko ya fahirisi ya bei ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani ulikuwa ni asilimia 10.8 mwaka 2012 ikifuatiwa na asilimia 9.2 kwa mwaka 2008. Kiwango cha chini ni asilimia 2.1 kwa mwaka 2011 kama inavyonekana kwenye kielelezo namba 1.

Kielelezo namba 1: Fahirisi za Uzalishaji wa Bidhaa za Viwandani (1985=100)



**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu
Ofisi ya Taifa ya Takwimu**